## Jibu la Uviko-19 barani Afrika:Pamoja kwa taarifa za kuaminika

### Ufafanuzi wa Maneno Kuhusu Haki za Binadamu

Uvunjaji wa haki za binadamu ni vitendo vinavyotekelezwa na mawakala wa serikali au watu ama kundi la watu kwa niaba ya serikali au kwa idhini waliyopewa na serikali, na ambayo inavunja haki za kimsingi za mtu.Vitendo hivi ni pamoja na kutiwa ndani na kuzuiliwa kiholela, pamoja na kutumia nguvu kupita kiasi.Ukiukaji wa haki za binadamu pia unaweza kutokana na serikali kushindwa kuwazuia watu wengine kutowanyima haki watu binafsi huku jibu la tatizo kama hili ikiwa ni ( kupitia uchunguzi wa kina wa visa kama hivi vya ukiukaji wa haki za binadamu, kutoa habari na kuwachukulia hatua wahusika kupitia vyombo vya kisheria).

Wakati wa uwepo wa janga la Uviko-19, wana-habari wengi walipigwa na maofisa wa polisi, wakatiwa mbaroni kiholela na haki zao nyengine zikavunjwa. Shirika la ARTICLE 19 limenakili visa kama hivyo katika nchi lengwa. Pia shirika hili limeweka ufafanuzi wa maneno yaliyotumika kuhusu kuelezea madhila waliyopitia wana-habari.

Mradi huu  umefadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya

**ARTICLE 19 Eastern Africa**

P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*

- **Kutiwa Mbaroni na Kuzuiliwa**




Hizi ni njia mojawapo za uvunjaji wa haki za binadamu zilivyoelezwa hapa.

**Kutiwa Mbaroni Kiholela**

1. Inapokuwa vigumu kuhusisha kitengo chochote cha sheria kumnyima mtu uhuru wake.
2. Mtu anapotiwa mbaroni bila kujali viwango vya kimataifa kuhusiana na kupewa haki ya kuwakilishwa kisheria au kuchukuliwa kuwa mshukiwa hadi mahakama itakapoamua.

3. Wakati kuzuiliwa kunapotekelezwa katika kuzuia, kwa mfano, maandamano ya amani na kuwazuia waandamanaji kwa kutekeleza haki yao ya kutoa maoni, uhuru wa kukutana na uhuru wa kutangamana na watu wengine.

- **Kupotezwa**





Kunaswa, kutiwa ndani, kutekwa au mbinu yoyote ya kunyima mtu uhuru wake inayotumiwa na maofisa/ au mawakala wa usalama, kundi la watu wanoafanya hivyo kwa idhini ya serikali, na kukana kukiuka haki za mtu kama huyo ambako kunamnyima uhuru wake na kuficha aliko mtu huyo, jambo linalomzuia mhusika kupata utetezi wa kisheria.

**ARTICLE 19 Eastern Africa**

P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*

- **Kushambuliwa kimwili/na mauaji ya kiholela**




Hivi ni vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu kwa kumdhuru mtu kimwili:

**Kutumia nguvu kupita kiasi**: kutumia nguvu kupita kiasi kunakofanywa na maofisa wa usalama ambako hakustahili kwenye kutimiza lengo la kumnasa mtu pasipo kuwa na hatari yoyote.


**Kutumia nguvu kusiko kwa lazima:** Huku ni kutumia nguvu kunakofanywa na maofisa wa usalama mahali ambapo lengo la kumnasa mhusika lingetekelezwa bila kutumia nguvu zozote.

**Mateso:** Inamaanisha kwamba maumivu makali iwe ya kimwili au kiakili yanapotekelezwa kwa kusidi la kupata taarifa kutoka kwa mhusika au mtu mwengine kwa ajili ya kumtisha au kumlazimisha kutoa taarifa kwa maofisa wa usalama.

**Mauaji ya kiholela:**

Hivi ni vifo vinavyotekelezwa maksudi na maofisa wa usalama au vikosi vyengine vya usalama.

- **Mashambulizi na Vitisho**




Hivi ni vitisho ambavyo vinajumuisha kudhuru mwili, ikiwemo kifo, iwe kwa moja kwa moja au kupitia mtu mwengine, vifaa vya mawasiliano kama simu au vitisho vya mdomo na mara nyingine kufikia kifo kwa mwana-habari mwenyewe, rafiki yake, jamaa ya familia au chanzo cha habari.Vitisho vya aina hii vinakuwa ni pamoja na kufuatilia nyendo za mhusika, simu za mara kwa mara za vitisho, usumbufu kutoka kwa maofisa wa serikali, matamshi ya maofisa wa serikali au polisi na shinikizo nyengine ambazo zinahatarisha usalama wa mwandishi habari katika kutekeleza majukumu yake.


**ARTICLE 19 Eastern Africa**


P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*

- **Sheria Finyu**




Hizi ni sheria au mabadiliko ya sheria au sera za serikali kuhusiana na kuwepo kwa Uviko 19 ambazo zinazuia haki ya kujieleza na kupata taarifa.

- **Waandishi wa Habari**





**ARTICLE 19 Eastern Africa**

P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*

Wana-habari /Waandishi habari ni watu ambao kazi yao ni kuchunguza, kutathmini na kusambaza taarifa mara kwa mara au kwa njia maalum, kupitia vyombo vya habari vya maandishi, vya kutangaza au vya kielektroniki( redia na televisheni). Kutokana na ujio wa njia tofauti za mawasiliano, uwana-habari umepanuka na kujumuisha watu wa kawaida ambao hawana ujuzi wa taaluma hii.

- **Taarifa za uongo**





Taarifa hizi ni zile ambazo kwa maksudi husambazwa ili kuzusha hofu katika jamii. [Soma zaidi kuhusu taarifa za uongo na uhuru wa kutoa maoni kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa.]

**ARTICLE 19 Eastern Africa**


P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*

- **Taarifa za Kupotosha**




Taarifa za kupotosha ni kusambaza taarifa za uongo bila kufahamu. [Soma zaidi kuhusu taarifa za kupotosha na uhuru wa kutoa maoni kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa].

- **Jinsi ya kupata taarifa**




Haki ya kupata taarifa au habari inampa mtu binafsi, makundi na kampuni au taasisi nyengine yoyote, haki ya kupata taarifa, stakabadhi au tarakimu kutoka ofisi yoyote ya umma bila ya kutoa sababu ya kufanya hivyo. Pia ni jukumu la maofisa wa serikali walioko kwenye ofisi hizo kufanikisha upatikanaji wa taarifa hizo kwa njia rahisi na kwa haraka. Soma maoni ya jumla kutoka umoja wa mataifa.

Kwa maelezo zaidi tembelea: www.article19.org/covid-19-response-inafrica

**ARTICLE 19 Eastern Africa**

P.O Box 2653 – 00100 Nairobi, Kenya |
Visiting address: Chaka Place, 3rd Floor, Argwings Kodhek Road
*Phone +254 727 862 230| Email: kenya@article19.org |www.article19.org*